**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 4 Barabara ya Ukaguzi, S.L.P 950, 411404 Tambukareli, Dodoma. Simu ya Upepo: "Ukaguzi"; Simu: 255(026)21612000; Tarakilishi: 255(026) 2117527,Barua pepe: ocag@nao.go.tz; Tovuti: www.nao.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Charles Edward Kichere leo tarehe 28 Machi, 2021 amemkabidhi Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ripoti za ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2020 katika hafla fupi iliyofanyika Ikulu Chamwino Jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Kitaifa wakiwemo Viongozi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Ripoti zilizowasilishwa kwa Mheshimiwa Rais ni kama ifuatavyo:

1. Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020;
2. Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali za Mitaa kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020;
3. Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020;
4. Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020;
5. Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa Kipindi Kinachoishia Tarehe 31 Machi, 2021;
6. Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia Tarehe 30 Juni, 2020;
7. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Usafi wa Masoko ya Vyakula;
8. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo ya Vituo vya Huduma za Afya Nchini;
9. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Miradi ya Ujenzi Kwenye Sekta ya Elimu inayotekelezwa kwa njia ya "Force Account";

10. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Uandikishaji na Utoaji wa Vitambulisho vya Taifa;
11. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Matengenezo ya Magari ya Serikali;
12. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mifumo ya Kudhibiti Ubora wa Vyakula Vinavyosindikwa Nchini;
13. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Mali Zilizotelekezwa;
14. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utekelezaji wa Udhibiti wa Uhamishaji wa Bei ya Mauziano ya Bidhaa au Huduma Baina ya Makampuni yenye Mahusiano;
15. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Ununuzi wa Pamoja wa Magari ya Serikali na Usambazaji wa Mafuta;
16. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Misamaha ya Kodi ya kwenye Miradi Ya Uwekezaji;
17. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Udhibiti wa Uchafuzi Unaotokana na Taka za Plastiki kwenye Bahari na Maziwa;
18. Ukaguzi wa Ufanisi Kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Awamu ya Pili ya Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Kasi Dar es Salaam;
19. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Usimamizi wa Udhibiti wa Mafuriko;
20. Ukaguzi wa Ufanisi juu ya Utekelezaji wa Mradi wa Uzalishaji Sukari wa Mbigiri; na
21. Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi Zilizofanyika na Kuwasilishwa Bungeni Mwaka 2016.

Akiwasilisha Ripoti hizo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Bwana Kichere alisema, “Mheshimiwa Rais, napenda kuishukuru Ofisi yako kwa kuniongezea watumishi wapya 25 kwa upande wa ukaguzi wa mifumo (TEHAMA) ambao wameongeza nguvu katika ukaguzi wa mifumo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2020”.

Aidha Bwana Kichere aliongeza kwa kusema, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imeweza kutumia mbinu mpya ya ukaguzi ambayo ni Real-Time Audit mbinu ambayo imesaidia kuongeza Ufanisi katika kaguzi zetu, ambazo mpaka sasa tumeweza kukagua miradi 6 kwa kutumia mbinu hii.
Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

1. Ujenzi wa Reli wa Kisasa (SGR) Dar es Salaam mpaka Makutupora
2. Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo kasi Dar es Salaam (BRT)-Gerezani-Mbagala
3. Upanuzi wa Barabara ya Morogoro kipande cha Kimara mpaka Kibaha
4. Mradi wa Uzalishaji wa Sukari Mbigiri
5. Mradi wa usambazaji maji katika wilaya ya Same, Mwanga na Korogwe
6. Ujenzi wa Mradi wa Umeme Julius Nyerere Hydro Power.

Baada ya makabidhiano hayo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu ameipongeza Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa kazi nzuri iliyofanyika kwa kuzingatia muda lakini pia ameiagiza Ofisi

hiyo kuendelea kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kulinda rasilimali za Taifa, na pia kutumia mfumo wa ukaguzi wa Real-Time Audit ili kufanya kazi kwa ufanisi Zaidi. “Naipongeza Ofisi ya CAG kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ukaguzi wa Nje wa Umoja wa Afrika kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka wa Fedha 2020-2021 kupitia mkutano wa 37 wa Baraza la Mawaziri wa Mambo ya Nje na Umoja wa Afrika uliofanyika Oktoba 2020 na pia kwa kuteuliwa kukagua Kamisheni ya Usimamizi wa Anga ya Afrika (African Civil Aviation Commission- AFCAC) yenye Makao yake Makuu Dakar-Senegal kwa miaka ya fedha ya 2020-2022.

Aidha Mheshimiwa Rais amemuagiza CAG kuhakikisha kuwa anaitumia vema fursa hiyo kwani ni sehemu ya kuwajengea uwezo watumishi wa Ofisi yake kwa ujumla na wakati huo huo amemtaka kufuatilia matumizi yote ya Fedha za Serikali kuanzia mwezi Januari mpaka Machi 2021.

Kwa Mujibu wa Ibara ya 143 kifungu kidogo 2 na 4 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa) kinamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kukabidhi Ripoti kwa Mheshimiwa Rais kabla au ifikapo tarehe 31 Machi kila mwaka na baada ya hapo Ripoti hizo huwasilishwa Bungeni ndani ya siku saba za mwanzo za kikao cha Bunge kinachofuata na baadae Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu huwasilisha taarifa zilizomo kwenye ripoti hizo kwa waandishi wa habari.

**IMETOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**